Chumba kinacho husika na ununuzi wa zahabu na alimasi

# Miaka 1990 na 1991 imeleta tumaini na nguvu ya kusonga mbele

**Kama kunako vitendo vitakavyobaki mda mrefu ndani ya vichwa vya watu kunako kazi za Benki ya Zaïre, kuumbwa kwa chumba chenyi kuhusika na ununuzi wa zahabu na almasi, ni moja kati ya vitendo vile. Kunako mwaka wa 1983, serkali yetu iliweza chukua hatua ya ku ruhusu ununuzi na uchuuzi wa zahabu na almasi nchini mwetu. Kwa sababu ya kuipiganisha uchuuzi wa magendo na wa uficho wa mali hayo. Ikiwa kama kwa mwanzo maduka iliyofunguliwa kwa kuuzishia zahabu na almasi zime weza tumika vizuri, kisha myaka michache, hasa mwaka 1989 mingi kati ya duka hizo sika funga milango. Na mwisho wa mwaka ule, mazao ya maduka hizo 6 ilikuwa tu ya 1200 kg ya zahabu. Wakati Benki imeona kama hali hiyo iliendelea kungandamiza uchumi wetu pahali pa hkuisimua, ika kusudia kujiingiza binafsi ndani ya soko ile, akiwataja viongozi na wa saïdizi wake katika kazi zile za mpya. Ni nini Benki ya Zaïre ilifikiri kuleta ya mpya hapo wafanyaviashara wa zamani walishindwa ? Walikuwa wakijiuliza watu wote. Kisha siku kidogo, jibu alikugawiya kuletwa na Benki ya Zaïre. Kisha mwaka moja wa kwanza ya kazi, kweli kabisa Benki ikaonyesha mfano mwema. Kutoka ku 1200 kg ya mwaka 1989 sawa vile mazao ya viwanda 6, mazao ya Benki mwenyewe ikafika ku 4300 kg. Mwaka wa pili, ma 1991, matoleo ya Benki ya Zaïre yakaongezeka, karibu 6000 kg kwa bei ya milioni 70 ya dola za kiamerika. Wakati huo, hesabu kutoka inchi huko zahabu ya Zaïre yauzishwa kwa magendo zimekuwa zenye kujulisha kama kila mwaka 12000 kg ya zahabu yauzwa kwao. Nikusema kama uwizi, uficho na kimagendo iliweza sana kukafirisha. Ni kwa iyo Benki ya Zaïre ikajipatia ukomo wa kukaribia kilo hizo 12000 ama sivyo kuzivuka. Kwa kweli isingelikuwa migorogoro ya siasa, magumu ya uchumi na wizi ama unyanganyi uliotukia kwetu, kama Benki ya Zaïre leo hii ingelipashwa towa mazao makubwa saana. Ingawa magumu ni mengi, Benki ya Zaïre, kufuatana na matunda aliyovuna kisha myaka miwili yale ya mwanzo, inajidaiya tu kusonga mbele. Magumu itapita tu, ila itafaa utaratibu saana kwani kama hali hiyo mbaya ikaendalea tu vile hakutakuwa hata namna ya kupanga oroza nyingine. Ni hivi basi, Benki ya Zaïre inatowa sauti kwa wale wote wanao wasaïdia katika kazi hiyo, awe wa duka la ununuzi ao awe mocimba zahabu ao tena mchuuzi ya kama inafaa kuendelea kumtegemea na kusahau kabisa kuvusha mali yetu kwa magendo sabaabu tunaharibu wenyewe uchumi wetu. Uwe pale Bukavu, uwe pale Kivu ya kaskazini, pale Zaïre ya juu, Shaba ao Maniema, fikirini vizuri.**

## Kwa nini Benki ya Zaïre kajiingiza katika soko ya zahabu ?

Jamhuri ya Zaïre sawa vile inchi zingine zote zinazo jitafutiya maendeleo, zinazo magumu sana ya kujipatiya feza za kigeni. Magumu inayoongezwa na malipo ya madeni za inje na kushuka kwa mazao ya mlimo na ya madini. Ubovu wa uchumi za inchi hizo yaongezeka tena kunyonywa kwa mali yao kimagendo ama kisirisiri.

Nchini kwetu Zaïre, sawa vile tulivyosema mbele, uwizi wa madini yetu ilituma serkali kuchukua mipango kunako mwaka 1983, lakini haikudumu. Zahabu na almasi zimeendelea tu kuvushwa na kuuzishwa mbali na mipaka ya Zaïre.

Tukumbushe kama mipango hiyo ilikuwa ina waruhusu wanainchi sawa vile wageni, kufungua viwanda vya ununuzi na uchuuzi wa zahabu na almasi popote nchini Zaïre kwa uchunguzi wa Serkali iliyokuwa mshauri wa Serkali kwa mambo. Benki ya Zaïre, mambo ya pesa na uchumi, ikaendesha mpango wake wa kusimika maduka ya umunuzi na uuzishaji wa madini yetu ghali kusudi ya kuipiganisha uwizi. Ni hivi, chini ya uongozi na uchunguzi wake akawakubaliya watu, sawa vile viwanda mbali-mbali, vyenye vilionekana kuwa vya kweli na vyenye kujitegemea majimboni huko wanako chimba madini yale.

Mwaka 1990 ikawa sawa vile mwaka wa kwanza wa uchunguzi na wa maanzisho ya kazi. Mazao ya mwaka·ule, ukashangaza saana watu wote. Benki yenyewe ikatoa kilo 4300 ya zahabu wakati mwaka 1989 uliyopita viwanda 6 vya zamani avikuweza kupita tarakimu ya 1200 kg. Furaha gani. Tumaïni likaongezeka na kazi zikaendelea.

Mwaka uliyofwata, ama 1991, mazao ikasonga tena mbele. Benki ikatoa kilo 6000 ya zahabu. Tujulishe kama ni pale Bukavu mji mkuwa wa Kivu ya zamani ndio Bendi ya Zaïre iliweza anzisha kazi zake za ununuzi na uchuuzi wa zahabu. Jimbo la Kivu ya zamani liliweza chaguliwa na Benki sababu kufuatana na hesabu zenye kuelekea madini, jimbo la Kivu ni lenye udongo unao zahabu kwa uwingi sawa karibu popote jimboni. Kuingia kwa Benki ndani ya soko hiyo, si kwa uyangu-yangu bali ni kufuatana na miandiko ya sheria ya inchi. Sheria hiyo, ina mwacha uhuru Benki ya Zaïre kuweza kutumikisha pesa za kigeni na kununua zahabu kusudi ya kuziuza inje ya Zaïre. Benki inaweza vile vile kuwataja wasaïdizi wake katika kazi zile. Ni kwa hiyo maduka kwa jina na kwa uongozi wa Benki ya Zaïre zika endelea kusimikwa majimboni. Mjini mkuu Kinshasa na jimbo la Zaïre ya chini, Kisangani mji mkuu wa jimbo la Zaïre ya juu, Bunia na Isiro huko huko tu Zaïre ya juu, Uvira na Bukavu, huko jimbo la Kivu ya kusini na pia Goma na Butembo huko jimbo la Kivu ya kaskazini.

Mipango na kazi za Benki ya Zaïre zikafurahisha sekali mpaka ikaombwa kwa Benki ya Zaïre kuendesha mipango kama zile kunako soko ya almasi. Lakini kufuatana na ukosefu wa noti za Benki mpango huo aukuharikishwa kama vile serkali ilikuwa ikitamani. Mwisho-mwisho, Benki ikatazama ginsi ya kuendesha kazi upande wa almasi. Tafauti kidogo ndani ya mpango huo. Kupewa kwa pesa ya Benki ya Zaïre kwa msaïdizi wake italingana na kutolewa kwa pesa za kigeni na msaïdizi huyo. Pia, kulazimishwa kwake kuonyesha kiasi ya pesa milioni 15 cha dola za kiamerika sawa vile pesa ya matumikio.

## Vyumba vya ununuzi jimboni

Kisha kufunguliwa kwa chumba cha ununuzi wa zahabu pale Bukavu, Benki ya Zaïre ikaendelea na kuzigundua popote huko nchini-Zaïre kupatinako zahabu. Chumba cha Kalemie kika funguliwa tarehe 17 yuni 1991 na kile cha Kisangani tarehe 2 septemba mwaka ule. Tueleze kama chumba cha Kisangani achikukua cha kwanza kufunguliwa ndani ya jimbo la Zaïre ya juu sawa vile Kalemie ilikuwa jimboni mwa Shaba. Huko Zaïre ya juu basi, viwanda viwili vianzisha kazi zile mbele saana ni Sonec na Ledor. Pa Kalemie katika Shaba, kufunguliwa kwa chumba cha ununuzi

*(Inafwata ukarasa 13)*